## Haki na Wajibu wa Mshiriki

Majina ya Washiriki wa WIC washiriki yaliythibitishwa leo:

### Haki Yangu

- **Vyakula vya WIC** : Nitapatiwa maelezo kuhusu kuhusu programu na jinsi ya kutumia ruzuku yangu ya WIC kwenye duka.
- **Huduma** : Wakala wa ndani watafanya huduma za afya, elimu ya lishe na kunyonyesha zipatikane kwa ajili yangu, na ninahimizwa kushiriki katika huduma hizi.
- **Taarifa za Huduma za Afya** : Nitapata taarifa kuhusu chanjo na huduma zingine ambazo ninaweza kuhitaji.
- **Utendewaji wa Haki** : Viwango vya kustahiki na kushiriki katika Mpango wa WIC vinalingana kwa kila mtu, bila kujali ya kabila, rangi, utaifa wa asili, umri, ulemavu, au jinsi.
- **Rufaa** : Nitashauriwa kwa maandishi ninapokuwa sistahiki kwa ajili ya WIC au nikiombwa malipo na ninaweza kuomba kusikilizwa kwa haki. Ninaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi wowote unaotolewa na wakala wa ndani kuhusu kustahiki kwangu kwa Mpango. Nina siku 90 kutoka tarehe niliyopokea notisi kwamba maombi yangu yamekataliwa , au ruzuku yangu imesitishwa ili kuomba kusikilizwa kwa haki. Ikiwa ruzuku yangu imesitishwa ni lazima niombe kusikilizwa kwa haki ndani ya siku 15 baada ya notisi yangu ya kusitishwa ili ruzuku yangu iendelee hadi mkaguzi anayesikiliza atoe uamuzi au muda wa uthibitisho uishe, chochote kitakachotokea kwanza.
- **Kipindi cha Uithibitishaji** : Nitaarifiwa angalau siku 15 kabla ya muda wa kila uthibitisho kuisha kwamba muda wa uthibitisho wangu unakaribia kuisha.
- **Heshima ya Kawaida** : WIC na wafanyakazi wa duka watanitendea kwa adabu na heshima. Niweza kuwaambia wafanyakazi wa WIC kwamba ningependa kutoa malalamiko iwapo hawakunitendea kwa heshima. Ninaweza pia kuwasilisha malalamiko kwa USDA katika anwani iliyo hapa chini.
- **Uhamisho Taarifa** : Iwapo ninahama, naweza kuhamisha taarifa zangu za WIC kwenye jimbo jingine. Ninaweza kuomba hati za uhamisho ili niende nazo.

### Wajibu wangu

Naelewa kwamba:

- WIC haitoi vyakula vyote au fomula zinazohitajika kwa mwezi na ruzuku ambayo haijatumika haiendelezwi hadi mwezi ujao.
- Ikiwa nitapoteza kadi yangu ya eWIC inaweza kubadilishwa. Ikiwa ruzuku yangu ya chakula itaisha muda wake kabla ya kupokea kadi mpya ya eWIC, ruzuku haitabadilishwa.
- Taarifa nilizozitoa kwa Mpango wa WIC Mpango zimewasilishwa pamoja na risiti ya Msaada wa Shirikisho. . Maofisa wa Mpango wanaweza kuthibitisha taarifa zinazotolewa kwao.

- Taarifa zinazomtambulisha mshiriki wa WIC zitatolewa kwa wale watu ambao moja kwa moja wanahusika na usimamizi, utekelezi na ukaguzi wa hesabu wa mpango.
- Katibu wa Idara ya Afya ya Pennsylvania anaweza kuidhinisha kuachiliwakwa taarifa zangu za WIC kwa mashirika ya umma ambayo yanahudumia watu waostahiki kwa ajili ya Mpango wa WIC, kama vile , such as Medicaid, the Supplemental Nutrition Assistance Program (SNAP), Temporary Assistance to Needy Families (TANF), the Maternal Mortality Review Committee (MMRC), Pennsylvania's Pregnancy Risk Assessment Monitoring System (PRAMS) na the Department's Division of Newborn Screening and Genetics (DNSG). . Mashirika hayo ya afya ya umma yanaweza tu kutumia taarifa zanguza WIC kwa ajili ya yafuatayo:
    - Ili kubaini kustahiki kwangu kwa ajili ya mipango yao na kurahisisha mchakato wa kutuma maombi
    - Kufanya uhamasishaji kwa ajili ya mipango hiyo.
    - Kuimarisha afya, elimu, au ustawi wa washiriki wa mipango yao na mpango wa WIC
    - Kupima na kutathmini Uitikiaji wa mahitaji ya huduma za afya ya Pennsylvania na matokeo.

I Nakubaliana kufuata ya sheria za hapo chini:

- Daima nitaleta ushahidi wa utambulisho wangu (Kitambulisho) kwa kila ziara ya kliniki.
- Nitatoa nyaraka zote zilizohitajiwa na Mpango wa WIC kwa wakati muafaka..
- Nitatumia vyakula na fomula ya WIC pekee kwa mtu aliyeko kwenye WIC.
- Niripoti kupotea, kuibiwa, au kuharibiwakwa kadi ya eWICk kama ilivyoelekezwa.
- Nitahikikisha kila mtu niliyemtaja kutumia ruzuku yangu anatambua Haki na wa Wajibu wa WICTumia Nitamfundisha kutumia ruzuku yangu a ipasavyo.
- Nitadumisha miadi yangu ya WIC au nitapiga simu kwenye kliniki kupanga upya. Iwapo nitashindwa kuchukua ruzuku yangu kwa mara tatu mfululizo naweza kuondolewa kwenye mpango..
- Sitauza, kugawa au kufanya biashara kadi yangu ya eWIC, vyakula, au fomula kwa pesa, mkopo, vocha za kubadilisha baadaye au vitu vingine. Ikiwa nina bidhaa za WIC ambazo siwezi kutumia, nitazirudisha kwenye kliniki.
- Sitachapisha bidhaa za WIC kwaajili ya kuuza au kufanya biashara kwenye mtandao.
- Sitaapiza, sitapiga kelele, e, sitanyanyasa, sitishia, au kureruhi kimwili wafanyakazi wa WIC au duka wafanyakazi, au kuharibu mali za WIC au duka.
- Sitamwandikisha mtoto ambaye hayuko chini ya uangalizi wangu kisheria. .
- Sitajiandikisha kwenye WIC katika zaidi ya jimbo moja au kupata ruzuku kutoka kwenye Kliniki ya WIC zaidi ya moja kila mwezi.

I Nakubali kutoa taarifa za kweli na zilizokamilika kuhusu:

- Utambulisho wangu, hali ya mimba na anwani.
- Idadi ya watu wote wanaoishi katika kaya yangu.
- Jumla ya vipato vya watu wanaoishi katika kaya yangu.

- Kuwa kwenye Medicaid,
- Pennsylvania Food Supplement Program (FSP), ambayo pia inajulikana kama Food Stamps au SNAP, au Temporary Cash Assistance (TCA).
- .
- Mabadiliko yote katika maisha (kwa mfano, Nitawajulisha WIC ikiwa nina mabadiliko kwenye kipato changu au ukubwa wa familia au kuhama).

Sahihi yangu kwenye mfumo wa WIC inamaana kwamba :

- Nimeshauriwa kuhusu haki na wajibu wangu chini ya Mpango.
- Nathibitisha kwamba taarifa nilizotoa kwa ajili ya kubaini ustahiki wangu ni sahihi, kwa kadiri ya ufahamu wangu. Fomu hii ya uthibitishaji inawasilishwa pamoja na risiti ya msaada wa Shirikisho. Maafisa wa mpango wanaweza kuthibitisha maelezo kwenye fomu hii.
- Ninaelewa kuwa kutoa taarifa ya uwongo au ya kupotosha kwa makusudi au kuwasilisha vibaya kwa makusudi, kuficha, au kuzuilia ukweli kunaweza kusababisha kulipa wakala wa Serikali, pesa taslimu, thamani ya ruzuku ya chakula niliyopewa isivyofaa na inaweza kunipelekea kuwa na kesi ya jinai au madai chini ya Sheria ya Jimbo na Shirikisho.
- Nimepewa, au nitapewa vifaa vya vhakula (kadi ya eWIC kadi) kwa ajili ya kaya yangu.
- Nimeuliza maswali yoyote niliyonayo kuhusu WIC, na yamejibiwa..
- Naelewa haki na wajibu wangu..
- Naelwa kwamba nikishindwa kufuata wajibu wangu kwamba nitakuwa sistahiki kuwa kwenye mapango wa WIC. .

Kwa mujibuwa Sheria za haki za kiraia za Shirikisho na kanuni za pamoja na sera za haki za kiraia haki sheria za Idara ya Kilimo ya Marekani (USDA) Mashirika yake, ofisi na wafanyakazi wake na taasisi zinazoshiriki au kusimamia programu za USDA haziruhusiwi kubagua kwa misingi ya kabila, rangi, asili ya kitaifa, dini, jinsi, ulemavu, umri, hali ya ndoa, hali ya kifamilia/ulezi, mapato yanayotokana na mpango wa msaada wa umma, itikadi za kisiasa, au kulipiza kisasi kwa sababu ya kushiriki kwenye shughuli za awali za haki za kiraia, katika programu yoyote inayoendeshwa au kufadhiliwa na USDA(si minsingi yote inatumika kwa programu zote). Sulihisho na tarehe za mwisho za kuwasilisha malalamiko zinatofautiana kulingana na programu au tukio. .

Watu wenye ulemavu wanaohitaji njia mbadala za mawasiliano kwa ajili ya kupata taarifa za programu (mfano , maandiko ya nukta nundu, maandiko yenye herufi kubwa, rekodi ya sauti, Lugha ya Ishara ya Marekani, n.k.) wanapaswa kuwasiliana na Shirika la Serikali ya Jimbo au la Mtaa linalosimamia programu hiyo au kuwasiliana na USDA kupitia Huduma ya mawasiliano ya Relay kwa kupiga 711 (sauti na TTY). Zaidi ya hayo, taarifa za programu zinaweza kupatikana katika lugha zingine mbali na Kiingereza.

Ili kuwasilisha malalamiko ya ubaguzi katika programu, jaza Fomu ya Malalamiko ya Ubaguzi wa Programu ya USDA, AD-3027, inayopatikana mtandaoni kupitia https://www.usda.gov/about-usda/general-information/staff-offices/office-assistant-secretary-civil-rights/how-file-program-discrimination-complaint na pia katika ofisi yoyote ya USDA, au andika barua iliyoelekezwa kwa USDA na uweke kwenye barua hiyo taarifa zote zinazohitajika kama zilivyo kwenye fomu. Ili kuomba nakala ya fomu ya malalamiko, piga simu kwa (866) 632-9992. Tuma fomu yako iliyokamilika au barua kwa USDA kupitia: (1) barua: U.S. Department of Agriculture, Office of the

Assistant Secretary for Civil Rights, 1400 Independence Avenue, SW, Mail Stop 9410, Washington, D.C. 20250-9410; (2) faksi: (202) 690-7442; au (3) barua pepe: program.intake@usda.gov .

USDA ni mtoaji huduma, mwajiri, na mkopeshaji mwenye fursa sawa kwa wote.